

Nini matatizo ya watoto Albino shuleni?

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ingawaje, akili zao hazina hitilafu watoto Albino mara nyingi hawafanyi vizuri shuleni, na huchukuliwa kuwa ni wajinga kwa sababu hawawezi kusoma vizuri ubaoni. Mara nyingi watoto Albino hujikuta wameaachwa katika shughuli za nje, ya madarasa zinazojumuisha wenzao shuleni. Walimu lazima watambue watoto Albino darasani mwao na wawe na mikakati maalumu wa kuwawezesha kufuatilia masomo. Wanafamilia pamoja na walimu shuleni wahakikishe kuwa Albino hawatengwi katika shughuli za vikundi. Kuwakutanisha na Albino wenzao au na watu wenye Albino kwenye familia zao na jamii kwa ujumla itawasaidia zaidi. Watoto Albino wanajifunza kufidia upungufu walionao wa kujithamini kwa kuweka jitihada katika masomo na shughuli nyingine. Wana mwelekeo wa kushinda zaidi katika mambo wanayojaribu. Watu weusi wengi wanaoishi na ualbino wamefanikiwa kuwa mafundi wazuri, wanasheria, wakunge wajasiriamali wataalamu wa kompyuta na hata maprofesa wa vyuo vikuu.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25431>